

MOSHI CO-OPERATIVE UNIVERSITY (MoCU) CHUO KIKUU CHA USHIRIKA MOSHI



MAHAFALI YA NNE (4) YA CHUO KIKUU CHA USHIRIKA MOSHI (MoCU)

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) anawatangazia wahitimu na wananchi wote kuwa Mahafali ya NNE (4) ya Chuo yatafanyika siku ya **Ijumaa, tarehe 07 Disemba, 2018** kuanzia saa 4:00 asubuhi kwenye Uwanja wa Michezo wa Ushirika. Mkuu wa Chuo Mhe. Pius Msekwa atatumuku Astashahada, Stashahada na Shahada kwa wahitimu.

Wahitimu watakaohudhuria sherehe za mahafali wanatakiwa kuthibitisha kwa **whatsapp au ujumbe mfupi wa maandishi**, kupitia namba **0715 462653** na barua pepe: dvca@mocu.ac.tz kabla ya **Ijumaa, tarehe 30 Novemba, 2018**.

Kila mhitimu atakayeshiriki ataazimishwa joho kwa gharama ya shilingi elfu thelathini tu (30,000/=) na litapatikana Chuoni siku ya **Jumanne, tarehe 04 Disemba, 2018 hadi Alhamisi tarehe 06 Disemba, 2018** kuanzia saa 3:00 asubuhi mpaka saa 9:30 alasiri. Mwisho wa kurudisha majoho ni siku ya **Jumanne, tarehe 11, Disemba 2018 saa 9:30 alasiri**. Faini ya shilingi elfu tano (5,000/=) itatozwa kwa kila siku itakayozidi. Malipo yafanyike kupitia MoCU Savings akaunti namba **01J2036991800** benki ya CRDB. Malipo yatumia "Control Number" zitakazotumwa kwenye akaunti za MUSARIS .

Mazoezi (rehearsal) kwa wahitimu yatafanyika katika Uwanja wa Michezo wa Ushirika **tarehe 06 Disemba, 2018** saa 8:00 mchana. Ambaye hatashiriki hatahudhurishwa. Cheti cha kuhitimu kitapatikana mara baada ya mahafali.

Mahafali yatatanguliwa na sherehe ya kutunuku tuzo (Prize Awarding Ceremony) itakayofanyika siku ya **Alhamisi, tarehe 06 Disemba, 2018** kwenye Ukumbi wa J. K. Nyerere kuanzia saa 3:30 asubuhi

WOTE MNAKARIBISHWA IMETOLEWA NA OFISI YA MAKAMU MKUU WA CHUO



Vision: To become a Centre of Excellence in Co-operative Education and Practice



Centre of Excellence in Co-operative and Business Management Training of the East Africa Community (EAC)